

**MAKALA: METHALI KAMA FOMULA KATIKA UTUNZI NA
UWASILISHAJI WA USHAIRI WA KISWAHILI: MFANO WA
BAADHI YA MASHAIRI YA ABDILATIF ABADALLA**

Na

**Joseph Nyehita Maitaria
Mwanafunzi wa Shahada ya Ph.D
Idara ya Kiswahili
Chuo Kikuu cha Kenyatta
Barua Pepe: nyehitam@yahoo.com**

Ikisiri

Makala haya yanatathmini matumizi ya methali katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Utunzi huu una historia ndefu na matumizi ya methali bado yanaendelea kutumiwa hata wakati wa sasa. Kwa kuzingatia methali, ushairi wa Kiswahili unaweza kuainishwa zaidi. Uainishaji huo ni kama vile, ushairi unaotumia methali nyingi na ule unaotumia chache. Watunzi hodari wa ushairi huu hudhihirisha zaidi ustadi wao kwa mizungu inayotokana na matumizi ya methali. Kwa hivyo, mwelekeo huu unaweza kuzingatiwa ili kuwadhihirisha wale ambao ni hodari katika matumizi ya methali moja au chache katika uwasilishaji wa tungo zao. Baadhi ya mashairi yanayopatikana katika diwani ya *Sauti ya Dhiki* (Abdilatif Abdalla) itarejelewa kama mifano. Hata yale mashairi ambayo hayana ithibati ya matumizi ya methali, mwanagwi wake huhisika au hutawala katika kazi zinayowasilishwa.

**METHALI KAMA FOMULA KATIKA UTUNZI NA UWASILISHAJI WA
USHAIRI WA KISWAHILI: MFANO WA MASHAIRI YA ABDILATIF
ABDALLA**

Na

Joseph N. Maitaria

Utangulizi

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na unaendelea kustawishwa kifani, kiumbuji na kimaudhui (Masinde 2003 na Wamitila 2002). Hali hii imetokana na dhima ya utanzu huu katika jamii za Afrika Mashariki zinazotumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano mapana na kitaifa. Kwa mfano, hapo awali, ushairi wa Kiswahili ulikuwa ukitungwa kimasimulizi na baadaye ukaanza kutungwa kimaandishi miongoni mwa jamii za waswahili zilizoishi katika upwa wa Afrika Mashariki. Kiswahili kilipoenea na kuwa maarufu katika mataifa ya Afrika Mashariki, ushairi wa Kiswahili ulitungwa kwa kuzingatia utamaduni na jamii pana (Gesero 2009). Kwa njia ya ubunifu, ushairi wa Kiswahili unakuwa ni nguzo ya kusawiria na kuwasilishia uhalisi wa maisha ya wanajamii katika miktadha mahususi ya kitamaduni.

Kadhalika, ushairi wa Kiswahili ulikuwa katika masimulizi na kuwasilishwa kama nyimbo au kughaniwa kisha baadaye ukaanza kutungwa na kuhifadhiwa kimaandishi (Babusa 2005 na Njogu 1993). Aidha, ushairi unapokaririwa au kusomwa kwa sauti unabainisha matumizi ya lugha ambayo ni ya kiwango cha juu cha usanii, hasa unapolinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili kama vile riwaya, hadithi fupi na tamthilia. Aghalabu, mshairi wa Kiswahili ana uhuru mkubwa katika matumizi ya ubunifu wa msamiati, uumbaji wa miundo mbalimbali ya kisintaksia pamoja

na tamathali za lugha. Kwa mfano Senkoro (1988), anakariri kwamba, kinachofanya maudhui kuwa muhimu katika ushairi wa Kiswahili ni uwasilishaji wake kupitia kwa ishara mahususi za lugha zinazojengeka katika tamathali za usemi. Kwa ujumla, sanaa ya ushairi wa Kiswahili uko katika uteuzi na mpangilio maalumu wa maneno. Kutokana na matumizi mahususi ya lugha na mbinu za uwasilishaji, ushairi wa Kiswahili huiathiri na kuigusa mioyo ya hadhira (Mulokozi na Sengo 1995). Kwa hivyo, utunzi na uwasilishaji wake hutegemea mno uwiano uliopo kati ya fani inayotumiwa na dhamira au maudhui yanayoibushwa na msanii.

Isitoshe, msanii anapotunga ushairi wake huathiriwa kwa kiwango kikubwa tajiriba lake linalofungamana na utamaduni wa jamii na mazingira yanayomzunguka. Kwa sababu hii, ushairi wa Kiswahili unapozingatiwa hubainisha kiwango fulani cha uhusiano mkubwa na jamii (Momanyi 1998 na Imbosa 1990). Katika mantiki hii, ushairi wa Kiswahili hupata umuhimu wake kutokana na jamii. Kimsingi, kunga za uwasilishaji na miundo ya lugha inayotumiwa na msanii huwa ni ile ambayo imeibushwa katika misingi ya utamaduni wa jamii husika. Methali kama kipengele cha lugha ya kimapokeo ya jamii, aghalabu hutumiwa mno katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili (Ligami na Barasa 2006). Hali hii inatokana na sababu kuwa methali ni misemo ya hekima na busara inayobuniwa na kutumiwa kimapokezi katika mawasiliano ya jamii. Kutokana na dhima yake ya kale katika jamii, methali zimeweza kutumiwa na kurithishwa kimasimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Ndungo 1998). Hivyo, methali inakuwa kiungo au kitoweo muhimu cha lugha ambacho hutumiwa katika

kuyatafakari na kuyapima maisha huku zikifichua falsafa na hekima ya jamii katika muktadha wa utamaduni maalumu (Gesero 2009:iv).

Kutokana na umaarufu wa methali katika mawasiliano ya jamii, baadhi ya wasanii wa ushairi wa Kiswahili walichelea kutozitumia kama kipengele mahsusi katika tungo zao (Kunemah 2008:ix). Mwelekeo huu ndio uliowaelekeza baadhi ya waandishi na wahakiki wa fasihi wa hapo awali kuchukulia kuwa methali ni ushairi mdogo wa Kiswahili (Knappert 1979). Mawazo hayo pia yameendelezwa kwa kiwango fulani na Mazrui na Syambo (1992) kwamba, matumizi ya vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili yalitokana na kuwepo kwa methali katika jamii.

Fauka ya hayo, mabadiliko mbalimbali yameweza kutokea katika Afrika Mashariki ambayo yameathiri mno mitazamo ya jamii kuhusu maisha na utamaduni wao. Methali nazo zinaendelea kutumiwa na baadhi ya wasanii wa ushairi wa Kiswahili wa kisasa kama nyenzo ya kuwasilishia maadili na kuhifadhia utamaduni wa jamii. Baadhi ya washairi wa Kiswahili waliotumia wingi wa methali katika usawiri wa tungo zao ni kama vile: Wallah (1988), Karama (1985), Mbega (1984), Uvetie (1983), Khan (1981), Amana (1982), Massamba (1976), Snow-White (1974), Abdalla (1973) na Nassir (1971).

Baadhi ya wasanii wa ushairi wa kisasa pia wameweza kutumia idadi ndogo ya methali katika diwani zao kwa kushirikisha arudhi za kimapokeo na mitindo ya mashairi huru. Baadhi ya watunzi wenye mwelekeo huu ni kama vile Khatib (2003), Mohamed (2002), King'ei (1999) na Mazrui (1994).

Katika mantiki hii, kuna uwezekano wa kuzingatia methali kama kigezo cha kuuainisha ushairi wa Kiswahili. Kwa hivyo kuna uwezekano wa kuwa na kitengo cha ushairi unaotumia methali nyingi, chache au moja katika utunzi na uwasilishaji wake. Makala hii inazingatia baadhi ya tungo za ushairi unaotumia methali zaidi ya moja. Aidha, inafafanua uwezekano wa kuainisha kwa ushairi wa kisasa wa Kiswahili unavyoweza kutokana na kutumia au kutokutumia methali katika tungo hizi.

Matumizi ya Methali Mbili au Zaidi Katika Shairi

Kikundi hiki cha ushairi kinaweza kushirikishi tungo ambazo zinatumia methali zaidi ya moja katika utunzi na uwasilishaji wake. Kitengo hiki cha ushairi tutakiita *Ukimembi*. Katika ushairi wa huu, matumizi ya methali mbili au zaidi ndani ya utungo hutokana kwa uelekezi wa anwani ambayo si methali. Ushairi huu unatofautiana na ule wa *Ukimea*¹ kwa ambavyo hautumii methali kama anwani (Taz. Shairi la ‘Mnazi Vuta N’kuvute’ uk. 17-22). Aidha, matumizi ya methali mbili au zaidi katika ushairi hujitokeza kiawamu au kwa kuzingatia mantiki mahususi kulingana na mahitaji ya mtunzi wa ushairi: mwanzoni (ya kwanza) katikati (ya pili, ya tatu au yoyote ile). Hapa ieleweke kuwa matumizi ya methali ya pili inaweza pia kuchukuliwa kuwa ya mwisho. Hata hivyo, methali ya mwisho inaweza pia kuwa ya pili kutegemea mfuatano wa kujitokeza kwayo katika uwasilishaji wa utungo. Methali ya mwanzo hujitokeza katika ubeti wa awali au katika beti za mwanzo endapo mshairi atakuwa anashughulikia hoja zaidi ya moja. Methali ya pili huweza kujitokeza katikati ya shairi au katika mojawapo ya beti za katikati endapo

¹ Ukimea: Ni jina linalowakilisha ushairi wa kiswahili unaotumia methali kama anwani katika utungo. Viambishi vilivyopigiwa mstari vimetumiwa kuundia jina hilo.

mshairi ametumia methali mbili au zaidi. Kwa hivyo, utungo unaweza kuwa na idadi yoyote ya methali katika uwasilishaji wake. Matumizi haya yanaweza kuwa ni ushuhuda wa ufundi au ujuzi alionao msanii katika umbuji na usarifu wa lugha. Shairi la Abdalla (1973:89-110) ‘Kutendana’, katika *Sauti ya Dhiki* linabainisha hali hii kama ifuatavyo:

MWANAMUME

kama bure utanipa, nipa sinisumbuliye

kama hutaki ‘takopa, nikulipe baadaye

Hivi sasa cha kukupa, sina; kweli nikwambiye

Mtu huwa hakutupa, amfaapo mwenziye (methali ya kwanza)

MWANAMKE

‘Sina’ kila siku ‘sina’, kwako I maisha

Huna siku utanena: ninacho ‘kanirambisha?’

Hiyo ‘sina’ yako Bwana, sasa ishanichokesha

Nyege ni kunyegezana, kwangu huba zinkwisha (methali ya pili)

MWANAMKE

Usemayo ni hakika, si urongo aswilani

Ni kwa kuwa nnachoka, kukufanyaa muhisani

Ndipo n’kabadilika, hakutowa maanani

Mjinga ‘meerevuka, mwerevu u mashakani (methali ya tatu)

Maelezo

Tamaa hakuitaka, akazidi bembeleza

Akasema yalopita, ni bora kunyamaza

Kuliko kuyafuata, na kisasi kulipiza

Yalopita yashapita, si vyema kuyaregeza (methali ya nne)

Methali kama kichocho cha kuibulia na kuwasilishia maudhui

Ujumbe unaowasilishwa katika shairi la ‘kutendana’ unahitaji kufafanuliwa kwa kuzingatia hoja za kichangamano. Hata hivyo, kinachobainika ni kwamba methali hizi zinashirikiana katika kuibua na kuendeleza zaidi ujumbe unaowasilishwa. Kwa mfano, mzoano baina ya Mwanamume na Mwanamke umepitia matukio mbalimbali hadi kufikia hali yake ya sasa. Hii ndio sababu ya msingi inayomfanya mshairi kutumia methali zaidi ya moja; kila moja inashikilia nafasi muhimu katika uchimuzi na udhihirishaji zaidi wa matukio. Katika methali ya mwisho, mshairi anajipa nafasi ya kutoa suluhisho la mgogoro uliopo.

Hata hivyo, kilicho cha muhimu ni kwamba, ushairi huu una methali ambazo zinaweza kuainishwa kuwa ya awali, ya ndani na ya mwisho katika uwasilishaji iwapo mtunzi anatomia methali zaidi ya mbili. Ikiwa msanii ametumia methali mbili, basi ile ya kwanza inakuwa ya awali na ya pili inakuwa ya hitimisho. Kinachodhihirika katika matumizi hayo ni kwamba, methali hizo huwa zinashikilia nafasi tofauti tofauti lakini zinashirikiana kimtindo na kuchangiana uwasilishaji wa ujumbe.

Methali ya kwanza inayojitokeza huwa ni ishara inayotanguliza ujumbe kwa mshindo lakini kwa matao ya chini. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi ni kwamba, mtunzi wa ushairi simulizi huuwasilisha utungo kwa ufahamu kuwa kauli zinazoshirikishwa hujitokeza kiawamu kama silaha ili mawazo yanayowasilishwa yaweze kutiririshwa kimantiki kuanzia mwanzo hadi mwisho (Propp 1968 na Lord 1960). Huu ni urasimi ambao pia unazingatiwa zaidi katika uwasilishaji wa tungo za ushairi wa Kiswahili unaozingatia arudhi za kimapokeo. Aidha, matumizi yake yanamfanya mtunzi kupata mwau wa kujenga muktadha au mandhari ya kijumla katika uwasilishaji wa utungo. Mathalani, muktadha unaoibushwa unaweza kuwa wa kihistoria au wa kijamii kulingana na uelekezo wa anwani ya shairi. Kwa mantiki hii, mshairi hana ulazima wa kutumia anwani yenye uelekeo wa methali. Kwa hivyo, methali hii inayotumiwa huwa ni kielekezi cha msingi kwa hadhira ya mshairi.

Kimsingi, idadi ya methali zinazotumiwa katika utunzi na uwasilishaji hutegemea idadi ya hoja au maudhui yanayosawiriwa. Katika muktadha huu matumizi huweza kuchukuliwa kuwa fomula ya utunzi ambapo hadhira hupata usuli wa mawazo yanayowasilishwa. Aidha, muundo wa shairi huweza kuibuliwa na kuelekezwa kupitia kwa methali hiyo inayotumika. Kwa ambavyo methali hii ya ‘mtu hakutupa, amfaapo mwenziye’ inajitokeza mwanzoni mwa shairi la ‘Kutendana’, inakuwa ni kauli ya msingi katika uwasilishaji wa utungo. Kadhalika, mshairi huwa na hadhari kubwa katika uteuzi wa methali hiyo inayotumika. Vile vile, methali ni ishara au matini mahususi ya lugha inayotawaliwa na inayojikita katika kanuni za kimuundo. Kisemiotiki, matumizi ya ishara za lugha sharti ihusishwe na muktadha wa ujumbe unaoibuliwa na kuwasilishwa

kwa wapokezi (Eco 1984 na Scholes 1982). Kwa hivyo, methali ya awali ndiyo inayopaswa kuumua zaidi ilhamu ya hadhira ili kuanza au kuendelea kulisoma shairi linalowasilishwa.

Matumizi ya Methali kama Mbinu ya Kuibulia Taharuki Miongini mwa Hadhira

Shairi linapokuwa na matumizi ya methali mbili, basi methali mojawapo inakuwa ya awali na nyingine inayotokea baadaye inakuwa ya tamati. Sawia na mwelekeo huu, mshairi anapotumia zaidi ya methali moja basi methali hizo zinaweza kujitokeza kwa awamu kama vile ya awali, ya kati na ya mwisho. Kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali, shairi linaweza kuwa na methali zaidi ya moja kutegemea idadi ya mawazo au hoja zinazowasilishwa. Kwa hivyo, si lazima shairi ambalo lina matumizi ya methali mbili liwe na matarajio ya uwepo wa methali ya tatu au zaidi.

Aidha, shairi linaposhirikisha methali mbili basi ya mwanzo hujitokeza awali na nyingine huwa ni kauli ya kuuhitimisha utungo. Kwa hivyo, endapo shairi lina methali mbili katika uwasilishaji wake, basi ile ya pili inajenga msingi wa kuendeleza wazo linaloibuliwa na methali ya awali au wakati mwingine inaweza kuibua hoja mpya ambayo inachangia zaidi hoja ya awali. Mantiki hii inajitokeza kwa uwazi kupitia kwa methali ya *Nyege ni Kunyegezana* katika shairi la Kutendana (uk. 89). Katika kiwango hiki, methali ya pili (au methali ambazo zinapatikana baada ya ile ya awali) inamfanya mtunzi kujenga msuko wa vitushi au mgogoro ambao unaibuliwa kitaharuki hadi kufikia kilele cha mgogoro wa vitushi. Endapo mshairi ametumia methali zaidi baada ya ile ya pili, basi methali hizo za baadaye kama vile, *Mjinga 'mervuka mwereu umashakani* (uk. 90) zitakuwa zinatenda

kazi sawia na ile ya pili lakini kwa kuendeleza na kufaragua zaidi kiini cha ujumbe unaowasilishwa kabla ya ile ya tamati.

Kadhalika, methali ya pili au ya tatu inapotumiwa mwishoni mwa beti za mwisho mwisho na shairi, utendakazi wake unakuwa ni kuhitimisha, kutoa suluhisho au kuielekeza na kuifanya hadhira kutafakari zaidi hoja muhimu zilizokwisha kuwasilishwa hapo mwanzoni. Katika mantiki hii, methali ya awali *mtu hakutupa, afaapo mwenziye* na ya tamati *yaliyopita yashapita, si vyema kuyaregeza* ndizo za msingi zaidi katika uwasilishaji wa utungo wa ushairi. Kwa sababu, mojawapo huwa inautanguliza ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa na nyingine inatamatisha mjadala katika utungo huo. Zaidi ya hayo, methali ya pili katika muktadha wa methali zingine huwa inajenga msingi wa taharuki na kuusukuma mbele ujumbe unaowasilishwa katika shairi.

Aidha, methali ya au za kati husaidia katika ubainishaji wa mkondo au mwelekeo wa mawazo yanayoibushwa na msanii. Mwelekeo unaochukuliwa na mtunzi aghalabu hujitokeza kwa uwazi zaidi katika kauli zinazopatikana katika beti za mwisho mwisho katika shairi. Kwa hivyo, taharuki inayojengewa hadhira inakuwa inachochewa zaidi kwa kuzingatia usaili na ufasiri na ujumbe unaowasilishwa (Gibbe 1995). Hii ni kwa sababu shairi huwa ni fumbo kutegemea umahiri wa mtunzi na kauli za msingi zilizotumika katika uwasilishaji wake. Isitoshe, kwa kuzingatia matumizi hayo ya methali, mshairi hataki hadhira yake isitishwe usomaji wake mwanzoni au katikati (pahali ambapo methali imetumiwa) bali hujengewa hamu ili iweze kuendelea kulisoma shairi lote ama kwa mwendo na mshindo unaostahili. Hapa ieleweke kuwa, matumizi ya methali ya pili

inayotumika katikati ya utungo humfunulia mwau msanii ili aweze kuvyaza wazo, hoja mpya au kuendeleza na kukuza kimakusudi mawazo ambayo tayari yalikuwisha kuwasilishwa hapo awali (Zingatia methali ya pili na tatu katika shairi la ‘Kutedana’). Kwa kutumia mifano tofauti tofauti inayotofautiana lakini inayopatikana au zinazotumiwa katikati baina ya ile ya awali na ya mwisho, inamsaidia au zinamsaidia zaidi mshairi katika kujenga na kuendeleza mawazo yanayoibushwa. Aghalabu, shairi linalowasilishwa kwa zaidi ya methali moja huwa ni utungo mrefu wenye beti nyingi kama vile inavyobainika katika utenzi. Kwa mfano, mtunzi wa shairi kama hili huwa anasawiri kisa kirefu chenya ujumbe au maudhui changamano ambayo yanahitaji kutolewa maelezo ya kina au mshairi anahitaji kujenga ushikamano wa mawazo tofauti tofauti na kuyawasilisha kwa mtiririko usiochosha au utaratibu unaostahili.

Kwa ambavyo mawazo yanayowasilishwa katika utungo ni mengi na changamano, huenda hadhira isiweze kufuutilizia kwa urahisi mkururo wa mawazo yanayoibushwa. Aidha, mshairi huyawasilisha mawazo hayo kiawamu huku akizingatia umbuji wa kauli teule zinazoshikamanisha mawazo na kulifanya shairi liwe na mtiririko usiomchosha msomaji. Kwa mujibu wa nadharia ya Fomula ya Kisimulizi, mawazo yanapasa kuwasilishwa kiawamu ili mtiririko uweze kudhibitiwa (Propp 1968). Hii ndiyo sababu ya kuwasilisha hoja tofauti tofauti katika utungo kupitia kwa mada ndogo ndogo. Msingi wa kufanikisha jambo hili ni kwa kuihusisha methali mojawapo kuwa kielekezi cha kufaragua zaidi hoja zinazowasilishwa. Jambo hili hurahisisha uwasilishaji, usomaji na upokezi wa ujumbe. Kwa hivyo, methali ya kati huteuliwa na hutumiwa kwa ustadi

mkubwa siyo tu kama mbinu ya kumdhibiti msomaji bali pia kama mbinu ya kuudhibiti mwendo wa kimahadhi katika uwasilishaji wa shairi.

Katika muktadha huu, methali ya kati huifanya hadhira kuwa na kipindi cha kupumua au kupata wasaa wa kuliajiri bongo ili kutafakari mawazo yanayoibushwa na pia kujiweka tayari kupokea mawazo mapya. Kimsingi, huu ni ujuzi wa msanii katika ujenzi wa utafakari ambao huifanya hadhira kusaili kila kauli msingi ambayo imetumiwa na mshairi katika uwasilishaji utungo. Mojawapo ya mbinu zinazotumika katika uelekezi huo ni methali iliyopo au zilizopo kama ilivyokwisha kuelezwa hapo awali methali hizo kiawamu katika uwasilishaji wa utungo. Kwa hivyo, mshairi anaweza kutumia mshabaha wa miundo ya kauli ya methali ya awali au kwa kuzingatia kauli za methali zinazofuatia ili kuundia mishororo katika shairi.

Shairi hili ni refu na lenye beti ambazo zinafanana au zinatofautiana kimuundo na kiumbo. Sawia na uwasilishaji wa utenzi, shairi hili husawiri maudhui ya kina na kwa uzingativu wa miundo tofauti tofauti ya lugha kulingana na tajiriba, ufundi au utashi wa mtunzi. Nayo methali ya mwisho, aghalabu hutokea kama kauli mwishoni mwa shairi. Hapa ieleweke kuwa, si lazima matumizi hayo ya methali yatokee kama kibwagizo au kiishilio.

Methali inayojitokeza mwishoni mwa shairi ina dhima ya kubainisha msimamo au mwelekeo wa mtunzi. Aidha, matumizi ya methali hii huufundika na vile vile huibulia muhtasari wa ujumbe ambao tayari umewasilishwa na umefafanuliwa kwa kina katika

beti zinazopatikana katika shairi kwa ujumla. Kwa mfano, methali *yaliyopita yashapita, si vyema kuyaregeza* (uk. 101) inashikilia nafasi ya nne. Kadhalika hii ndiyo ya mwisho katika uwasilishaji wa shairi. Vile vile, matumizi ya methali hii huifanya hadhira kupata ishara au dira ya uelekezi na utafakari wa kijumla kuhusu mawazo yanayowasilishwa hasa kwa kuyapatanisha na tajriba ya maisha katika jamii. Kulingana na nadharia ya Semiotiki, kauli au ishara inayotumika kaitika mawasiliano ya watu hupata ufasiri wake kwa kuzingatia utamaduni wa jamii (Barthes 1981 na Hawkes 1977). Kwa njia hii, mawazo ya mtunzi husaki na kuacha athari kubwa katika akili ya msomaji wa shairi.

Sifa bainifu za ushairi unaotumia methali zaidi ya moja katika uwasilishaji

Kutokana na maelezo yaliyozingatiwa kuhusu matumizi ya methali zaidi ya moja katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili, utungo huu unaweza kuwa na sifa za msingi kijumla zifuatazo:

- Matumizi ya methali zaidi ya moja zinaweza kutumika katika utunzi na uwasilishaji wa shairi. Hii ni kwa sababu, shairi huweza kuwa na dhamira na maudhui ndogo ndogo.
- Ushairi wa kisasa wa Kiswahili unaweza kushirikisha miundo mbalimbali ya lugha kutegemea uelekezo wa inayotumika au zinazotumika katika utunzi na uwasilishaji wake.
- Mawazo ya mtunzi husawiriwa na huwasilishwa kwa kuzingatia mbinu ya taharuki.

- Ushairi wa Kiswahili huwasilishwa kwa kuzingatia mtiririko au utaratibu maalumu ambapo kuna mwanzo, kati au ufaraguzi zaidi wa ujumbe na hitimisho.
- Mawazo ya mshairi, iwapo ni ya kichangamano, yanaweza kusawiriwa na kuwasilishwa kwa kina kwa kuzingatia shairi refu.
- Mwendo, ridhimu na mahadhi hudhibitiwa katika uwasilishaji wa shairi.
- Uwasilishaji wa shairi hujenga uhusiano mkubwa kati ya mtunzi na hadhira.
- Utunzi na ufaraguzi wa mawazo katika ushairi hupata mwelekeo kutokana na methali zinazotumika.
- Mfumo wa mizani na urari wa mizani huweza kubadilika kutegemea uelekezi wa methali zinazotumika.
- Uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili huzingatia fomula maalum.

Kwa kuzingatia mashairi katika diwani ya *Sauti ya Dhiki*, sifa za ushairi wa *Ukimembi*² zinabainika zaidi katika mashairi yafuatayo:

- Shairi la *Zindukani* (uk. 69-72)
- Shairi la *Kutendana* (uk. 89-110)

Hitimisho

Katika uchanganuzi wa baadhi ya mashairi katika diwani ya ‘*Sauti ya Dhiki*’ inabainika kuwa methali zina nafasi muhimu katika utunzi na uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili

² Ukimembi: Ni jina linaowakilisha ushairi wa Kiswahili unaotumia methali mbili au zaidi katika utungo. Viambishi vilivyopigiwa mstari vimetumiwa kuundia jina hilo.

hata wakati wa sasa. Kwamba, matumizi ya methali yanaweza kuwa angavu zaidi au matumizi yake huweza kudhihirika kama mwangwi wa kurejelea ujumbe unaowasilishwa.

Kigezo cha matumizi ya methali nyingi kinachotumika katika uainishaji wa kundi hili la mashairi ya Kiswahili kinaweza kushirikisha maudhui yanayoibushwa, miundo, maumbo na mitindo ya utunzi, vipengele vya utamaduni vinavyorejelewa katika ufasiri wa ujumbe na mabadiliko ya kiwakati yanayoshuhudiwa katika jamii. Kwa hivyo, matumizi ya methali yanaweza kutumiwa katika kuuanisha utanzu wa ushairi wa Kiswahili kwa kuzingatia fani inayotumika katika uwasilishaji na maudhui yanayoibushwa. Aidha, matumizi ya methali zaidi ya moja katika uwasilishaji, hubainisha umahiri na uhodari wa msanii. Pia, kuna uwezekano wa matumizi haya ya methali kutumiwa kuwa mbinu ya kuelewa viwango vya umbuji wa watunzi: wale waliobobea zaidi na wale ambao ni bado wanagenzi au wanaochipukia katika mbinu za uwasilishaji katika tungo za ushairi wa Kiswahili.

MAREJELEO

- Abdalla, A. (1973): "Ushairi wa Kiswahili na Uhuishwe Usiuliwe", katika *Zinduko*. Dar es Salaam: Jarida la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Babusa, H. O. (2005): "Vigezo badilia kuhusu uanishaji wa Mashairi ya Kiswahili", Tasnifu ya M. A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Barthes, H. O. (1981): "The Theory of the Text", Ian Macleod (Mt.), katika Young, R. (Mh.), *Untying the Text*. London. Routledge.
- Eco, U. (1976): (1984): *Semiotics and the Philosophy of Language*. London: Macmillan Press Limited.
- Gesero, W. C. (2009): *Methali za Kiswahili Afrika Mashariki na Kati*. Dar es Salaam: Absit Co.
- Gibbe, A. G. (1978): "Fasihi na Jamii: Baadhi ya Washairi wa Kiswahili, 1960-77", katika *KISWAHILI* Juzuu 48/1 Dar es Salaam: TUKI.
- _____ (1980): *Shaaban Robert: Mshairi*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- _____ (1990): "Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili", katika Gibbe, A. G. (Mh.) *Jarida la KISWAHILI, Juzuu 1*. Dar es Salaam: Education Services Centre.
- _____ (1995): "Inkishafi: Uhakiki wa Kidayakronia", Tasnifu ya Ph. D. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)
- _____ (1998): "Sajili ya Ushairi", katika Gibbe, A. G. (Mh.), *Mwongozo wa Ushairi Na. 1*. Mashairi ya Taria. Eldoret: SEKUKI.
- Gibbe, A. G. na Mvungi, T. A. (1987): *Fasihi kwa Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: Standard Publishing Company.
- Hawkes, T. (1977): *The Structuralism and Semiotics*. London. Methus.
- Imbosa, R. (1990): "Jazanda katika Ushairi wa Muyaka", Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Khatib, M. S. (1999): "Tamathali za Usemi", katika MULIKA Na. 25. Dar es Salaam, TUKI.

- King'ei, G. K. (1982): "Uhakiki wa *Nthimo* (Methali) za Kikamba kwa Kufuatisha Misingi ya Methali za Kiswahili". Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- _____ (1994): "Swahili Taarab as a Medium of Political Expression in Kenya", katika *Writers Forum*, a Journal of the Writers' Association of Kenya. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation Publishers and Printers.
- _____ (2000): *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- _____ (2007): "Athari za Washairi Wakongwe juu ya Washairi wa Kisasa: Mfano wa Muyaka bin Haji na Ahmed Nassir", katika *Kioo cha Lugha*, Juzuu la 5. Dar es Salaam: TUKI.
- King'ei, G. K. na Kemoli, A. (2001): *Taaluma za Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- King'ei, G. K. na Kisovi, C. M. (2005): *Misingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- _____ (2000) "Stunted Growth of Kiswahili Literature: Causes and Remedy", katika *KISWAHILI Juzuu 63*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kisia, A. na Mwarandani, B. (2007): *Uketo wa Ushairi kwa Shule za Upili Ukijumlisha Utungo wa Diwani Yetu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Knappert, J. (1979): *Four Centuries of Swahili Verse: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann.
- Kunemah, A. S. K. (2008): *Misemo na Methali katika Ushairi*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Ligami, P. na Barasa, S. (2001): "Tahakiki ya Methali za Kiswahili", katika Njogu, K., Momanyi, C. na Mathooko, M. (Wah.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Taweza Communications.
- Lord, A.B. (1960): *The Singer of Tales*. Cambridge: Harvard University Press.
- Masinde, E. (2003): "Ushairi wa Kiswahili Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui". Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Mazrui, A. (1988): *Chembe cha moyo*. Nairobi. Heinemann Kenya Ltd.

- Mazrui, A. na Syambo, B. K. (1992): *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi. East African Educational Publishers.
- Mbaga, N.O. (1978): Dhima ya Ushairi Katika Kuhifadhi Historia ya Jamii”, katika *MULIKA Na. 14*. Dar es Salaam. TUKI.
- Mbughuni, P. (1978): “From Oral to Written Literature: The Politicization of Kiswahili Literature”. Tasnifu ya Ph.D, Bloomington. Indiana University. (Haijachapishwa)
- Momanyi, C. (1988): “Ushairi wa Mwanamke Muislamu katika Jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili”, Tasnifu ya Ph.D., Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Mulokozi, M.M. na Sengo, T.S.Y. (1995): *History of Kiswahili Poetry*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- Ndungo, C. (1998): “Image of Women in African Oral Literature: A Case of Gikuyu and Swahili Proverbs”. Tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)
- Njogu, K.(1993): “Dialogic Poetry: Contestation and Social Challenge in East African Poetic Genres” Tasnifu ya Ph.D, Chuo Kikuu cha Yale. (Haijachapishwa)
- Propp, V. (1968): *Morphology of the Folktale*. Austin: University of Texas Press.
- Scholes, R. (1982): *Semiotics and Interpretation*. New Haven: Yale University Press.
- Senkoro, F. E. M. K. (1988): *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.
- Wamitila, K.W. (2002): *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.